September, 2019

# JARIDA LA ATD DUNIA YA NNE TANZANIA

***"KUSHIRIKIANA PAMOJA ILI KUWAWEZESHA WATOTO, FAMILIA NA JUMUIA ZAO KATIKA KUTOKOMEZA UMASKINI ULIOKITHIRI."***

## TAHARIRI



Ndugu wapendwa,

Ni matumaini yangu kuwa ni wazima wa afya na mnaendelea vizuri katika harakati za mapambano dhidi ya umaskini uliokithiri. Nasi hapa ATD Dunia ya nne tunaendelea na harakati pamoja na kuhakikiksha shughuli zote zinaendelea tukianza na maadhimisho ya siku ya kutok- omeza umaskini uliokithiri duniani tarehe 17 Oktoba 2019 Kamati ya maandalizi inaen- delea na maandalizi ya maadhimisho hayo yatakayofanyika katika ukumbi wa chuo cha ufundi stadi cha Don Bosco kilichopo oyster- bay ikisindikizwa na kauli mbiu isemayo "kushirikiana kwa pamoja kuwezesha watoto, familia na jumuiya zao katika kutokomeza umaskini." Pia tunaendelea na shughuli za maktaba ya mtaa, ambapo inaendelea kuwezeshwa na vijana wa ATD Dunia ya nne, katika kuboresha wawezeshaji wamekuja na wazo la kuwapeleka watoto maktaba ya taifa kwa ajili ya kujisomea. Hii inawafanya watoto kupenda kusoma vitabu na watoto wameipokea vizuri.

Baada ya kufanya utatifiti kwa miaka mitatu Kuanzia mwaka 2016 hadi 2019, mradi huu wa kubaini vipimo vya umaskini ume- hitimishwa mwezi juni 2019 kwa kufanya kikao kikubwa na wadau mbalimbali kwa ajili ya mawasilisho ya vipimo na kuitambulisha mbinu mpya ya utafiti ya kuunganisha maarifa (MoK). Pia kwa mwezi uliopita kulikua na matukio kadhaa ikiwemo semina ya vijana ililyofanyika nchini Rwanda iliyo- husu mafunzo ya Tapori. Huu ni mtandao wa mawasiliano wa watoto ambao huwaleta wa- toto pamoja na kubadilishana uzoefu na maarifa ya watoto kutoka sehemu mbalimbali duniani kote. Pia kulikua na semina iliyohusu masuala ya fedha, semina hi ilihusisha wafan- yakazi wawili wa kudumu wa ATD Dunia ya nne. Mafunzo hayo yameweza kuwajengea uwezo mkubwa katika utunzaji wa fedha na maadili yake.Vilevile vijana wawili walikwen- da kwenye semina huko makao makuu Ufa- ransa. Semina hiyo ilihusu mawasiliano, kama tunavyojua mawasiliano ni kitu muhimu kati- ka mwenendo wetu ili kujua taarifa kutoka makao makuu na kutoka katika maeneno mengine duniani kote.

Tumekuwa na upungufu wa wafanyakazi w kudumu wa ATD dunia ya nne hapa kwetu Tanzania baada ya wafanyakazi wawili ku- hamishiwa makao makuu Ufaransa, hili ni jambo la kawaida kiutendaji na lengo ni ku- kujifunza na kufanikisha shughuli za ATD Dunia ya nne.

Tunatumaini utafurahia kusoma jarida letu.

Venance F. Magombera

*Siku ya Kimataifa ya Umoja wa Mataifa ya Kutokomeza Umasikini 2019* **UJUMBE WA SIKU**

*Dhima — " Kushirikiana pamoja ili kuwawezesha watoto, familia na jumuia zao katika kutokomeza umaskini uliokithiri."*



Mwaka huu unaweka kumbukumbu ya miaka 30 ya kupitishwa kwa Mkataba wa Haki za Mtoto (UN-CRC) mnamo 20 Novemba 1989. Mkataba huu wa haki za binadamu unaweka wazi haki za raia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na haki za kitamaduni kwa kila mtoto, bila kujali kabila lao, dini au uwezo wao.

Mkutano huo mahususi unatambua haki ya kila mtoto ya kuwa na kiwango bora cha kuishi kwaajili kumtosheleza kwa mtoto, kimwili, kiakili, kiimani na kimuhemko. Umasikini huathiri maendeleo ya watoto na husababisha kipato na afya duni ukubwani. Wakati umasi- kini kwa watoto unapotambuliwa kama ukatili wa haki za watoto za kibinadamu basi watu walio katika nafasi za madaraka wanawiwa kisheria kuhamasisha, kulinda na kutimiza haki za watoto. Zaidi ya yote, ni muhimu kutambua na kushughulikia ubaguzi wanaopitia watoto wa kike.

Watoto lazima watambuliwe kama watendaji kamili kwa ustawi wao badala ya kuwa vitu vya



uchaguzi tu vilivyowekwa kwa niaba yao. Kwa kweli, ushiriki wa watoto ni moja wapo ya kanuni za msingi za UNCRC, ambayo inahimiza kwamba watoto na vijana wana haki ya kutoa maoni yao kwa uhuru na kushiriki na kupata taarifa zote muhimu zinazohusiana michakato ya kufanya maamuzi inayoathiri maisha yao.

Ushiriki unaweza kutokea katika ngazi mbalimbali ambapo watoto wanaweza kutoa ufahamu ambao wengine hawawezi kutoa. Ushiriki wa watoto lazima uwe wa kimfumo, muundo na vifaa vya kutosha ili uwe na maana na ufanisi.

Kimsingi, maoni ya watoto, haswa sauti za watoto walio katika mazingira magumu, zinapaswa kusikilizwa na kuchukuliwa kwa uzito katika maendeleo ya sera na mikakati madhubuti ya kuzuia na kumaliza umaskini wa watoto. Wakati watoto na vijana wanajifunza kuwasilisha maoni, kubeba jukumu na kufanya maamuzi, wanaendeleza hali ya umiliki, haki, uwajibikaji na mshikamano.

"*Namna gani kulinda haki za wa- toto bila kulinda haki za wazazi? Hatuwezi kuongea kuhusu watoto bila kuongea kuhusu wazazi wao na familia... ni kama mti, wazazi ni mizizi na watoto ni matawi. Lazima kuwajali watoto lakini kwaajili ya wazazi pia, ili mizizi iwe imara.*"Ujumbe kutoka ATD Dunia ya Nne Montreal , Canada.

Ushiriki wa watoto unaweza kutambuliwa kikamilifu wakati serikali inatimiza majukumu yake, na familia na jamii zinawezeshwa vya kutosha kupitia fursa na mipango madhubuti ya kupunguza umasikini ili kuwawezesha kuunda mazingira ya salama na yenye kukuza ambapo watoto wanaweza kutambua uwezo wao kamili na kwa uhuru ku- tumia haki zao za kibinadamu. Mada ya mwaka huu inatukumbusha kwamba juhudi zetu za kuondokana na umasikini lazima zishughulikie utimilifu wa haki zote za watoto kama ilivyoainishwa katika UNCRC. Utoto ni wakati maalum katika maisha ya kila mtu. Ni wakati ambao watoto wanapaswa kutiwa moyo kujifunza, kucheza na kukua kimwili na kiakili na familia zao na jamii iliyoenea ya watu wazima katika mazingira salama na yenye kujali. Ujumbe wa kukuza utoto ni jambo muhimu katika kuendeleza kizazi kijacho chenye afya.

Lakini, leo ukweli kwa mamilioni ya watoto ni kwamba wananyang'anywa haki ya utoto ya msingi. Pasipo wao kuwa na kosa, watoto wanaishi katika umaskini na wananyimwa haki zao za kuishi, afya na lishe, elimu, ushiriki, na ulinzi dhidi ya hatari, unyanyasaji na uba- guzi. Kwa hawa mamia kwa mamilioni ya watoto ambao wanakabiliwa na unyonge wa kila siku wa umaskini, ahadi ya utoto iliyowekwa kwenye Mkataba wa Haki za Mtoto haijafikiwa kikamilifu.

Ajenda ya Umoja wa Mataifa ya 2030 inaweka msingi wa kupunguza umasikini na kuhakikisha kuwa hakuna mtu anayeachwa nyuma. Sehemu muhimu ya juhudi za kumaliza umaskini ni utekelezaji wa mifumo ya kinga ya kijamii ambayo inajumuisha na kushughulikia mahitaji, kujali na haki za watoto na familia zao. Hivi sasa, watoto wengi wanaoishi katika umaskini hawalindwi na ulinzi wa kijamii. Kuinua watoto na familia kutoka katika umasikini na kukuza ushirikishaji wa jamii na uwezeshaji, tunahitaji kupanua wigo wa usalama wa jamii, na hakikisha umeundwa vizuri, unafadhiliwa ipasavyo, unapatikana kwa wote wanaohitaji, kutosha kukidhi mahitaji ya msingi.

Hata hivyo, sera za serikali pekee haziwezi kuunda ushiri- kishaji wa kijamii na majadili- ano ya kijamii ambayo ni ya msingi katika kuwafikia wale walioachwa nyuma zaidi na kukabiliana na umaskini katika hatua Nyanja zake zote. Kwa mfano mtandao wa watoto wa Tapori, unaonyesha njia muhimu ambazo watoto wanaweza kukusanyika pamoja ili kujiimarisha wenyewe kushiriki vema zaidi katika familia zao na jamii kama wajumbe wa mabadiliko. Hatua kama hizo lazima ziungwe mkono na kutiwa moyo na serikali na jamii kama vijenzi vya msingi vya ushiri- kishwaji wa jamii.

Ni muhimu kwamba ushiriki wa watoto utambuliwe kama mchakato na sio tukio la mara moja. Mashauriano ya mara kwa mara hukosewa kwa kudhaniwa ni ushiriki.Wakati mchakato wa mashauriano una- kusanya maoni ya watoto juu ya suala fulani au swali, ushiri- kiinamaanisha kwamba wato- to wanajiunga katika kufanya maamuzi.

Maadhimisho ya Oktoba 17 kila mwaka yanaonyesha jinsi tunavyoweza kufanikiwa zaidi kwa kuwezesha watu kutoka pande zote za maisha kukusanyika ili kuheshimu haki za binadamu na umati wa watu wanaoishi katika umasikini. Ushiriki wa watoto na vijana umekuwa ukitiwa moyo na kuungwa mkono kama sehemu muhimu ya maadhimisho ya Oktoba 17 katika Umoja wa Mataifa na ulimwenguni kote. Hii inatambua majukumu muhimu ambayo watoto wanaweza kufanya kwa kushiriki na kutumia maarifa muhimu waliyoyapata kutoka kwa mapambano yao ya kibinafsi ya kila siku ili kuushinda umaskini.

Iliadhimishwa tangu 1987 kama Siku ya Ulimwengu ya kushinda Umaskini uliokithiri na kutambuliwa na Umoja wa Mataifa mnamo 1992, Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Umasikini inakuza mazungumzo na kuelewana kati ya watu wanaoishi katika umasikini na jamii zao, na jamii kwa jumla. "Inatoa nafasi ya kutambua juhudi na mapambano ya watu wanaoishi katika umasikini, nafasi kwao kufanya maswala yao kusikika na nafasi ya kutambua kuwa watu masikini wako mstari wa mbele katika vita dhidi ya umasiki- ni." (Umoja wa Mataifa , Ripoti ya Katibu Mkuu, A / 61/308, para. 58)

Habari zaidi juu ya mipango, hafla na shughuli za kuweka kumbukumbu ya Oktoba 17 kote ulimwenguni zinaweza kupatikana kwenye tovuti: overcomingpoverty.org na UN-DESA.

Kamati ya Kimataifa ya Oktoba 17

12, rue Pasteur F-95480 Pierrelaye, Ufaransa

http://www.over ezayopoverty.org

**MAKTABA YA MTAA TANDALE NA MAKTABA YA TAIFA**

Kwa kipindi kirefu tumekuwa tukiendesha shughuli za maktaba ya mtaa katika maeneo ya Tandale katika mtaa wa Pakacha. Lengo la maktaba ya mtaa ni kuwa karibu na familia zinazoishi katika umaskini uliokithiri na kuwapa nafasi watoto katika jamii lakini pia kuleta ukaribu kwa watoto wanaotoka katika hali tofauti za kiuchumi na kuwafanya wote wajione sawa.

Katika kuboresha shughuli za maktaba ya mtaa tuliamua kuwapeleka watoto Maktaba ya Taifa ili waweze kujifunza zaidi kupitia vitabu mbalimbali vya hadithi vyenye mafunzo mbalimbali.
Na pia huwa tunashirikisha wazazi katika safari hii ili nao waweze kujumuika pamoja na watoto wao katika safari hii ili nao waweze kuifahamu Maktaba ya Taifa na kile ambacho watoto wanakwenda kujifunza.
Wazazi na watoto wanafurahia sana safari hii yenye mafunzo ndani yake kwani watoto na wazazi wanapata fursa ya kujifunza.







Awamu ya kwanza ya utafiti ilihitimishwa mwezi Juni 2019. Mnamo mwezi Mei 2019, baadhi ya wanatimu ya utafiti walihudhuria katika mkutano uliofanyika jijjini Paris. Mkutano huo ulifanyika tarehe 10 Mei makao makuu ya OECD.

Mnamo mwezi Mei 2019 tarehe 26, mkutano wa wadau ulifanyika katika kituo cha Aliance France. Idadi ya mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya maendeleo, wasomi na wawakilishi kutoka katika mashirika ya kimataifa yali- wakilishwa. Washiriki walichangia maoni yao kuhusiana na matokeo ya utafiti. Hivi karibuni matokeo haya yatawakilishwa katika Ofisi ya Takwimu ya Taifa



TAPORI

Mnamo mwezi Julai mwaka 2019 baadhi ya vijana kutoka katika kundi la vijana wa ATD Tanzania walishiriki semina ya Tapori iliyofanyika nchini Rwanda.

Semina hii ilihusisha vijana kutoka nchi mbalimbali za Afrika.

Lengo la semina hii lilikua ni kwanza vijana kujua ni namna gani Tapori huendesha shughuli zao, changamoto na mafanikio katika shughuli zao.

Pili kuwezesha vijana kubadilishana uzoefu walionao katika kuratibu shughuli mbalimbali za kijamii hasa zinazohusu watoto.

Vijana waliweza kupata mbinu mpya ambazo wengine huzitumia katika kuratibu shughuli maktaba ya mtaa na Tapori.



Semina iliyohusu masuala ya fedha na maadili yake ilifanyika mjini Kigali nchini Rwanda mnamo Julai 30 hadi tarehe 2 Agosti 2019. Semina hii ilikuwa imeratibiwa na PAEFI (Pole Administration, Ethics International Financing) kwa kushirikiana na Shirika la Rwanda la Umuseke. Kwa ushirikiano wao semina iliwaleta pamoja washiriki kutoka nchi mbali mbali za Afrika ambazo ni; Burkina Faso, Senegal, Cameroon, Afrika ya Kati, Tanzania, Burundi, Rwanda na Kenya. Katika semina hii washiriki walifanyia kazi masuala yaliyohusiana na vyanzo vya fedha ndani ya shirika la ATD, maadili na kufanya maamuzi katika matumizi, ufadhili wa miradi na ufuatili- aji, utoaji wa taarifa za fedha na zana zake, ushirikiano wa ndani na wa kimataifa.

Semina ilihitimishwa kwa kutembelea eneo la kumbukumbu ya mauaji ya kimbari ya Kitusi mjini Kigali katika nchi ya Rwanda.

**SEMINA YA MAWASILIANO**

Emma Mahengo na Elizabeth Makata waliondoka kuelekea Ufalansa kuhudhulia semina fupi ya mawasiliano na kushiriki katika kambi ya vijana .waliondoka tarehe 1 Julai 2019 na kurejea tarehe 18 Julai 2019

Wakati wa semina ya mawasiliano walishirikishwa, kubadilishana na kujifunza mambo mengi kuhusu mawasiliano kutoka kwa washiriki wengine hasa nchi hizo kama vile Guate- mala, ambazo zinafanya vizuri zaidi katika sekta hiyo.

Katika kambi ya vijana walijiunga na vijana kutoka nchi nyingine, walifanya mambo tofauti pamoja kama vile kufanya ukarabati, uchoraji na kutengeneza paa la ofisi ya Fr.Joseph. Kukaa pamoja ili kuwezesha vijana kutoka nchi mbalimbali kushiriki, kubadilishana uzoefu kwa kujadili masuala pamoja na hivyo kujifunza mambo mengi kutoka kwa kila mmoja na kuishi kama familia.

**Taarifa kutoka kwa Timu ya ATD Dar es Salaam, Tanzania.**

Kuanzia mwishoni mwa mwezi wa Nne mwaka huu kikosi cha wanaharakati wa kudumu katika timu ya ATD Dunia ya Nne Dar es salaam kimezidi kupungua baada ya wanaharakati wawili wa kudumu Laurent Ganau pamoja na mkewe Alexie Gasenga- yire kuomba kuungana na timu nyingine huko Ufaransa. Ingawa tulipenda waende- lee kuwa nasi ili tuendelee kupata mchan- go wao, maarifa yao jitihada zao za kuhakikisha kwamba harakati za ATD Tan- zania zinasonga mbele hapa Tanzania, lakini kutokana kuhitajika zaidi mchango wao huko Ufaransa ilibidi waondoke ili kuongeza nguvu katika timu nyingine .

Na hii ni kawaida katika maisha ya wana- harakati wa kudumu huwa hawakai se- hemu moja kwa muda mrefu ili kutoa fursa kwa wangine kufunza na kushirikisha mawazo mapya na maarifa mapya lengo ni kuhakikisha kwamba shughuli za ATD Dunia ya Nne zinaendelea kwa mafani- kio. Tunachukua fursa hii kukumbushana kuwa ATD Tanzania ni ya Watanzania na Watanzania ndio wenye jukumu la kuhakikisha kwamba harakati zinasonga mbele na kuimarika zaidi . Kwa sasa timu ya ATD Tanzania ina wanachama wa kudu- mu watatu ambao ni Hemed A. Hemed, Salma Avith Mosha na Salehe M. Seif na Pelagie Mukampamira ambaye amekubali Kuungana nasi na kuchukua jukumu la kushirikiana nasi katika shughuli za kiuta- wala ili kutoa fursa tuweze kutekeleza ma- jukumu yetu kwa wepesi zaidi katika kuzifikia familia zinazoishi katika mazingira magumu yaliyokithiri. Hivyo tunaomba ushirikiano wenu wa karibu na wadhati ili harakati zetu zizidi kushamiri hapa Tanza- nia za kuhakikisha kwamba kusudio letu la UTU wa kila mtu unathaminiwa na kuhesh- imiwa linatimia.

**Wasiliana nasi!**

ATD DUNIA YA NNE—SLP 6786—DAR ES SALAAM

Namba ya Ofisi: 022761717 Atd.tanzania@gmail.com

Kiswahili website:http://ww.atd-fourthword.org/where-we-are/africa/tanzania/tanzania/ Ukurasa wa Facebook: https://www.facebook.com/atd.duniayanne